

CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



S.L.P. 1125, DODOMA Simu: 026- 2961101 Fax: 026 -2961100,
Barua Pepe: info@lgti.ac.tz Tovuti: www.lgti.ac.tz

MWONGOZO WA KUFANYA MAOMBI YA KUJIUNGA NA CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA

Taarifa muhimu kwa wanaotarajia kutuma maombi ya kujiunga na masomo kwa mwaka 2021/2022 katika ngazi ya Astashahada (Certificate), Stashahada (Diploma), Shahada (Bachelor Degree).

KOZI ZINAZOTOLEWA:

1. Utawala katika Serikali za Mitaa (Local Government Administration)
2. Usimamizi wa Rasilimali Watu (Human Resource Management)
3. Maendeleo ya Jamii (Community Development)
4. Uhasibu na Fedha katika Serikali za Mitaa (Local Government Accounting and Finance)
5. Utunzaji wa Kumbukumbu (Records, Archives and Information Management)
6. Ugavi na Ununuzi (Procurement and Supply Management)

SIFA ZA WAOMBAJI

1. Astashahada ya Awali (NTA Level 4 - Basic Technician Certificate)

Sifa: Mwombaji awe amepata angalau ufaulu wa "D" 4 za Kidato cha Nne(CSEE). Masomo ya Dini hayahusiki.

2. Astashahada (NTA Level 5 -Technician Certificate)

Sifa: Mwombaji awe amepata angalau ufaulu wa "Principal Pass" moja na "Subsidiary" katika mtihamu wa Kidato cha Sita (ACSEE) AU awe na Astashahada ya Awali (NTA Level 4 Certificate) kutoka Chuo chochote kilichosajiliwa na kutambuliwa na Serikali (na matokeo yake yawe yamepelekwa NACTE). Pia awe amepata angalau ufaulu wa "D" 4 za Kidato cha Nne(CSEE). Masomo ya Dini hayahusiki.

3. Stashahada (NTA Level 6 - Diploma)

Sifa: Mwombaji awe na Astashahada (NTA Level 5-Technician Certificate) toka Chuo chochote kilichosajiliwa na kutambuliwa na Serikali.

4. Shahada (Bachelor Degree)

- i. Shahada ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Bachelor Degree in Local Government Administration and Management).
- ii. Shahada ya Maendeleo ya Jamii (Bachelor of Community Development).

Sifa: Mwombaji awe na ufaulu wa Kidato cha Sita wa **Principal Pass mbili zenye jumla ya pointi 4.0** au awe na Stashahada (Diploma-NTA level 6) yenye GPA isiyopungua 3.0 katika kozi husika.

ANGALIZO:

Kama mwombaji amefanya mtihani wa kidato cha nne zaidi ya mara moja na kufaulu, aambatanishe nakala za vyeti vyake vya awamu zote za mitihani alizofanya.

NAMNA YA KUFANYA MAOMBI

Maombi yote yanafanyika kwa njia ya mtandao (**Online Application System**) kupitia tovuti ya Chuo www.lgti.ac.tz

Mwombaji anatakiwa kuandaa taarifa zifuatazo kwa ajili ya kuzitumia wakati wa kufanya maombi kwa mtandao (**ONLINE APPLICATION SYSTEM (OAS)**):

- i. Namba ya mtihani wa kidato cha nne au cha sita
- ii. Mwaka wa kuhitimu kidato cha nne au sita.
- iii. Ada ya maombi Sh 10,000/= (iwe kwenye *Mpesa, TIGO Pesa, HaloPesa, Airtel Money nk.*) itakayolipwa baada ya kupata **CONTROL NUMBER** kwenye mfumo.
- iv. Tarehe ya kuzaliwa ya mwombaji
- v. Namba ya simu ya mwombaji
- vi. Shule ya msingi aliyosoma
- vii. Wilaya ambako shule ya msingi iliko.
- viii. Namba ya simu ya mzazi au mlezi
- ix. **KOZI** unayotaka kusoma.

KUMBUKA:

- i. Maombi ya Astashahada na Stashahada (Certificate and Diploma) yatafunguliwa kwa kufuata **Kalenda ya Udahili ya NACTE** kuanzia mwezi Mei 2021 hadi Septemba, 2021.
- ii. Maombi ya Shahada (Bachelor Degree) yatafuata **Kalenda ya Udahili ya TCU**.

Tarehe rasmi ya kuanza kupokea maombi itatangazwa kupitia tovuti ya Chuo www.lgti.ac.tz

Kwa maelezo zaidi piga simu namba **0755 241 010** (Piga Jumatatu hadi Ijumaa saa za kazi, kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri).

KARIBUNI SANA!

